

# Pambazuko

Toleo Namba 029

Jumatatu Januari 30- Feb. 05, 2023



**Mbossa  
kuipa  
msukumo  
mpya TPA**

Uk. 5

**Samia kuvuna  
kura za vijana,  
wanawake,  
wapinzani**

Uk. 4

● *Ni katika uchaguzi wa 2025*

**Mwalimu aliyechapa  
nyayo yamkuta**

Uk. 6

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye  
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

## **Happy Birthday Rais Samia**



**U**ONGOZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa), wafanyakazi, waandishi wa habari na wachangiaji wa gazeti la Pambazuko wanapenda kumtakia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza miaka 63 tangu kuzaliwa kwake.

Tuna imani kwamba Mungu amempa uwezo wa kuongoza, kuleta faraja na amani kwa wananchi na kwamba karama hiyo hatakubali kupokonywa kwa kiburi cha madaraka, ukuu wala sifa anazopata kila uchao.

Gazeti la Pambazuko linamtakia heri na mafanikio yenye kuacha alama kwa uongozi wake ambao unaaminika kubeba taswira ya kujali, kuthamini na kutenda haki kwa kila mmoja bila kubagua wala kuwa na chembe ya uonevu.

Kila jema kwako Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na uzao wako.



Aliyekuwa mgombea urais wa Tanzania 2020 kupitia Chadema, Tundu Lissu aliwasili Dar es Salaam, Januari 25, 2023 baada ya kuwa nje ya nchi kwa zaidi ya miaka miwili. Aliondoka Tanzania kwa hofu ya usalama wake. Lissu ni makamu mwenyekiti wa chama hicho cha ushindani. Picha ya Reuters.

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## **NUKUU**



“Kuuzeza umma kwamba shule moja imeongoza kwa ufaulu katika mitihani, huenda tulikuwa tunatangaza na kuifanyia biashara shule hiyo, shule zipo nyingi zaidi ya elfu 18, sasa unapotaja moja sidhani kama ina tija.” – Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania, Athumani Salumu

---

## Samia kuvuna kura za vijana, wanawake, wapinzani

Na Waandishi WETU

**Z**IPO kila dalili kwamba Dkt. Samia Suluhu Hassan, atagombea nafasi ya urais anayoishikilia sasa katika uchaguzi mkuu ujao – miaka mitatu kutoka sasa.

Mbali na “kufokea” waliozusha kwamba hatagombea na yeye mwenyewe kueleza kwamba atawania nafasi hiyo katika uchaguzi ujao, tayari marais (wastaafu); Jakaya Kikwete na Ali Hassan Mwinyi wametamka mara kadhaa kwamba “hawaoni mtu wa kuchuana na Samia ndani ya chama na hata kwa wananchi.”

Ni kutokana na msingi huo, chama tawala - Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambamo yeye ni mwenyekiti wake, kimepata mgombea wake wa urais 2025.

Pamoja na kupata mgombea wake, CCM na serikali yake – na kupitia kwa Rais Samia mwenyewe, kuna mchakato wa kuhakikisha kwamba kura nyingi za ushindi wa kiti cha urais zinapatikana kutoka kwa wapigakura watakaokuwa na sifa za kushiriki uchaguzi huo.

Tayari Rais Samia na wasaidizi wake; ndani ya chama na serikali wamebaini eneo ambalo lina kura nyingi, eneo la vijana na wanawake, hasa wale walioko maeneo ya vijijini wenye ajira kubwa juu ya ardhi; kilimo.

Hawa ni vijana na wanawake na sasa Rais Samia, pamoja na kutimiza wajibu wake, amebaini fursa ya kuwapa “mbeleko” ili wamkumbuke na kumpa ridhaa ya kuongoza Tanzania, safari hiyo - akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyechaguliwa kwa sanduku la kura.

Rais Samia alingia ikulu Machi, 2021 baada ya kufariki kwa rais aliyekuwa madarakani, John Pombe Magufuli. Wakati wa utawala wa Rais Magufuli, Samia alikuwa makamu wake.

Wachambuzi wa siasa na uchaguzi wanadai kwamba Rais Samia kuwekeza



Trekta

zaidi kwa vijana na wanawake, anajiwekea mazingira mazuri ya “kubeba” kura nyingi za kumpa nafasi ya kuendelea kuongoza Tanzania.

Dkt. Lenny Kasoga akizungumza na Pambazuko anaeleza kwamba Rais Samia ameona mbali na kwa hakika anapenda kuendelea kuongoza, ndiyo maana anafanya kila analoweza kuhakikisha kundi kubwa la wapigakura wanapewa kipaumbele kwanza.

“Uzuri wa Mama Samia, kwa kufanya hivyo anatekeleza wajibu wake, lakini pia anajenga uwanja utakaobeba hao anaonekana kuwahudumia zaidi kwa kuwawezesha, sayansi ya siasa na uchaguzi, inaonekana anaicheza vyema sasa,” anaongeza Dkt. Kasoga ambaye ni mhadhiri mstaafu wa vyuo vikuu mbalimbalmali ndsani na nje ya Tanzania.

Dkt. Kiondo Kalunga, mkurugenzi wa taasisi mpya ya Kivuli anaeleza kuwa Rais Samia “amechagua” fungu jema la kuhakikisha vijana, tena wasiokuwa na ajira za uhakika, wanaingia shambani na kupata ajira muhimu, hivyo hawawezi “kumsahau” kitapakujua kipindi cha

## **Mbossa kuipa msukumo mpya TPA**

**Na Mwandishi WETU**

**M**AMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imepania kuendelea kudhihirisha kuwa ni kitovu cha kutunisha mfuko wa mapato ya serikali (Hazina).

Lengo la kupania huko ni kuhakikisha kwamba huduma zinaboreshwa zaidi, kusikiliza wateja na kuongeza nguvu ya ari ya wafanyakazi kuwajibika zaidi kwa weledi na uzalendo uliotukuka.

Matamano hayo, ambayo mengi yameanza kufanyiwa kazi, yameelezwa na Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa katika nyakati tofauti; akiwa na waandishi wa habari, wageni wanaojifunza utendaji wa mamlaka hiyo na katika mawasilisho kwenye mikutano na makongamano.

Mbossa anaeleza kuwa TPA kwa sasa nguvu kubwa zinaelekezwa kujitangaza zaidi kwa kueleza kuwepo kwa ufanisi na mazingira bora kwa wateja wa bandari, hasa zile kubwa zinazotumiwa zaidi na wafanyabiashara ama serikali za nchi jirani. Nchi hizo ni pamoja na Burundi, Rwanda, Zambia, Malawi na hata Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mkuu huyo wa TPA anaeleza pia mipango ya kutumia mawakala na kufungua ofisi katika maeneo mbalimbali, hasa nje ya nchi ili kuwapa wateja wao nafasi ya kupata huduma kwa urahisi na uhakika zaidi.

Kutokana na kuanza kwa maboresho hayo, huku mengine yakiendelea kufanyiwa kazi, tayari kuna matokeo chanya ambayo yamerekodiwa kwa kipindi kifupi baada ya kuanza kwa mabadiliko hayo.

Katika kipindi cha miezi sita, taarifa za TPA zinaonyesha kwamba mamlaka hiyo imeweza kuvuka lengo lake la kupokea na kusafirisha mizigo katika bandari zake. Kwamba kuanzia Julai hadi Desemba 2022 mamlaka hiyo imevuka lengo kutoka kuhudumia mizigo tani milioni 10.8 hadi milioni 12.1.



*Plasduce Mbossa*

Mbali na mizigo hiyo, pia katika kipindi hicho, meli zinazotia nanga katika bandari za TPA zimeongezeka na kuvuka lengo; kwamba ilitarajiwa kuwepo kwa meli 2214, lakini kuna ongezeko la meli 614, na sasa zimefikia meli 2828.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) ina fursa nyingi na uwezo mkubwa wa kuwzesha utekelezaji wa majukumu yake ya kuhudumia nchi zilizo jirani zinazohitaji msaada wa bandari kama lango la kuingia na kutoka kimataifa. TPA ina jukumu muhimu katika ukanda wa Afrika Mashariki ya kutoa huduma za bandari kwa nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ( DRC), Zambia, Uganda, Rwanda na Burundi.

“Bandari za TPA zikiwemo za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ziko katika maeneo yenye kurahisisha kupokea wateja wengi zaidi, endapo kutakuwepo ufanisi, kukomesha ucheleweshaji na upotevu wa mizigo,” anashauri Boaz Kiromo na kujibiwa na Mbossa kwamba mambo hayo yamefanyiwa kazi nanndiyo maana mafanikio yameanza kuonekana.

Bandari ya Dar es Salaam ni mlango mkuu unaunganisha Tanzania, majirani na nchi nyingine duniani kote na kwamba nguvu kubwa zinaelekezwa katika kuimaridha miundombinu yake.

---

**Mwalimu aliyechapa nyayo yamkuta****Na Scovya MANASE**

**S**ERIKALI mkoani Kagera imeomba radhi kwa umma na kuchukua hatua ya kumsimamisha kazi mwalimu anayeonekana akiwaadhibu wanafunzi kwa kuwachapa fimbo kwenye nyayo.

Mwalimu huyo, Isaya Benjamin Emmanuel aliyekuwa Mkuu wa Shule ya Msingi Kakanja, Wilaya ya Kwerwa, Kagera, amechukuliwa hatua hiyo na mkuu wa mkoa huo, Albert Chalamila.

Januari 10, 2023, mwalimu huyo anaonekana kwenye video akiwachapa wanafunzi wawili kwenye nyayo.

Aliwachapa viboko kwenye nyayo wakiwa wameketi sakafuni na kunyoosha miguu, huku akiikanyaga ili wasiweze kujitikisa.

Wanafunzi waliochapwa ni Salmon Kakwezi wa darasa la nne, mwenye umri wa miaka tisa; na Anord Kweyamba wa darasa la nne pia, mwenye umri miaka kumi.

Pambazuko limeelezwa kuwa mwalimu huyo aliwachapa viboko wanafunzi hao kwa sababu hawakufanya kazi ya nyumbani waliyopewa wakati wa likizo.

Chalamila alitangaza taarifa za kusimamishwa kazi kwa mwalimu huyo, Januari 24, 2023. Tayari imeundwa tume kuchunguza tukio hilo ili kuona kama kuna sababu za kumpeleka mwalimu huyo mahakamani.

Tukio hili ni sehemu ya mtiririko wa ukiukwaji wa miongozi ya serikali kuhusu namna ya kutoa adhabu za kimwili kwa wanafunzi (corporal punishments.)

Mwaka 2018, mwalimu mwanafunzi wa darasa la tano, Speri Eradius Patrick wa Shule ya Msingi Kibeta, Manispaa ya Bukoba, Kagera, anadaiwa kumpiga na kumuua mwanafunzi wa darasa la tano, Speri Eradius.

Siku moja baadaye, mwanafunzi wa sekondari ya Kalangalala mkoani Geita, Jonathan Mkono, alipigwa na mwalimu Lawson Lechipya, mpaka kuzimia na kulazwa hospitalini.



*Albert Chalamila, Mkuu wa mkoa wa Kagera*

Mwaka 2016, katika shule ya Sekondari ya Kutwa ya Mbeya, mwanafunzi alipigwa na walimu watatu mpaka akakimbia shule.

Mwaka 2016 tena, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Mbogamo ya Njombe, alipigwa na walimu wake mpaka kupoteza fahamu.

Na mwaka 2013, mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Mkwakwani, mkoani Tanga, alimpiga viboko mwanafunzi wake mpaka kumsababishia mguu kupooza.

Wanafunzi wote hawa wamekuwa wakipigwa kutokana na tuhuma za utovu wa nidhamu wa aina tofauti.

Tanzania inazo kanuni zinazotaja utaratibu mzuri wa kusimamia nidhamu ya wanafunzi shuleni. Yaani, kanuni za kudhibiti “adhabu za mateso ya kimwili” (corporal punishments) shuleni za mwaka 2002.

Kanuni hizi zilitangazwa kupitia gazeti la serikali namba 294; The Education (Corporal Punishment) Regulation, Government Notice No. 294 of 2002.

Kanuni hizi zinatoa mwongozo unaoonyesha aina, kiwango na wakati wa kutoa adhabu stahiki za mateso ya kimwili kwa wanafunzi shuleni.

Hata hivyo, Pambazuko linatambua kuendelea kuwepo kwa uvunjaji mkubwa kwa walimu kufuata kanuni za kutoa adhabu, ndiyo maana matukio ya wanafunzi kuimizwa kwa adhabu za viboko yamekuwa yakiongezeka.

## Wakenya wanogesha ‘birthday’ ya Samia

Na Tryruckia MFINANGA

**H**APA duniani kuna hatua tatu muhimu katika maisha ya kila mtu; kuna kuzaliwa, kuigiza katika filamu ya “maisha” inayochezwa kwenye jukwaa liitwalo dunia, na kuondoka jukwaani ama kwa njia ya kifo au wenye imani - kwa kupalizwa mbinguni.

Kwa kipindi cha miaka 63 iliyopita, Samia Suluhu Hassan, amekuwa anaigiza katika jukwaa hili katika nafasi mbalimbali za mchezo wa maisha. Kwa sasa yuko katika nafasi ya upeo; akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ijumaa ya Januari 27, 2023 ilikuwa kumbukizi ya miaka 63 tangu kuzaliwa kwake.

Watu mbalimbali, ndani na nje, vikiwemo vyombo vya habari, walimtumia salamu za pongezi kwake. Idadi kubwa ya wananchi wa Kenya hawakubaki nyuma, kama ambavyo video fupi zilizosambaa katika mitandao ya kijamii zinaonyesha.

Profesa PLO Lumumba, mwanasheria na mtetezi mkubwa wa asili ya Afrika kutoka Nairobi, Kenya alisikika alfajiri ya Ijumaa akimpongeza na kumtakia mema Rais Samia katika kukumbuka siku ya kuzaliwa kwake.

Lumumba anasikika akisema; “tunakutakia mema, tunakushabikia, umethibitisha kwamba una uwezo wa kuchapa kazi kwa misingi ya kizalendo, na wote tunakubali unachapa kazi kama mwanademokrasia halisi, na ama kweli nyota njema huonekana asubuhi.”

Hatimate, Lumumba akawasihi Watanзания wasimwangushe katika uchaguzi ujao wa 2025, kabla ya kusema dua ifuatayo kwa Rais Samia; “tunakuombea uwe katika mstari wa mbele tunapohamasisha harakati za kuleta muungano katika sehemu hii ya Bara la Afrika, na hatimaye kuunganisha Afrika kisiasa, kiuchumi na kijamii.”

Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi, waliongoza wanafunzi wengi



**Rais Samia Suluhu Hassan**

wa vyuo vikuu katika jiji hilo la Kenya walikusanyika ukumbini kuadhimisha kumbukizi ya kuzaliwa kwa Rais Samia. Wavulana kwa wasichana, wanapokezana kinasasauti na kutamka maneno ya kumpongeza Samia.

Msemaji wa kwanza anasema; “Samia ni menta mzuri;” wa pili anatamka; “Samia ni nembo ya viongozi wanawake, ametia fora;” wa tatu anaeleza; “Samia amenipa hamasa ya kuanza kujiandaa kuwa rais mwanamke wa Kenya;” wa nne anaongeza; “Samia ni kiongozi shupavu.”

Aida Odinga, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Spector, huko Nairobi, alisema; “ujumbe wangu kwa Samia ni kwamba, wewe ni nembo ya Afrika, unatupa fahari kuwa wanawake katika Afrika, wanawake wengi tunakushabikia, wewe ni mfano wa kuigwa kwetu.” Aida ni mke wa kiongozi wa upinzani Kenya Raila Odinga.

Na hapa Tanzania, watu binafsi na vyombo vya habari kadhaa vilirusha salamu za pongezi kwa Rais Samia, ikiwemo redio na luninga. Huku wasanii wakitawala zaidi salamu hizo za pongezi kwa Rais Samia.

## Haki ni chemchem ya baraka

**Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA**

**J**E, safari ya kusimamia na kutenda haki ilikuwaje ndani ya jamii yetu katika mwaka 2022?

Hakuna jambo la hatari na ambalo hunyang'anya amani na furaha ya kila raia katika taifa kama kuvurugika kwa mfumo wa utoaji haki.

Hali ya jinsi hiyo inapokuwepo katika jamii husababisha maumivu na machungu mengi yanayobeba machozi na hata kumwagika damu za watu wasiokuwa na hatia.

Kuvurugika kwa mifumo ya utoaji haki kunatokana na nguvu ya uovu, hujeruhi vibaya utu wetu wa asili. Biblia inatuambia kuwa tayari utu ule wa asili ulikwisha vurugwa na ibilisi kupitia kwa njia ya Adamu na Hawa.

Kwa imani ya kikristo, ukombozi katika Kristo uliliponya jeraha alilotutia shetani, lakini kovu lingalipo (fundisho la Baba wa Kanisa Askofu Augustino wa Hippo). Kwa kifupi tumepewa nguvu za kushinda uovu kwa nguvu ya ukombozi wa nafsini alionifanyia Kristo.

Pale ambapo neema haitupi ushindi dhidi ya uovu, basi ni muhimu iwepo sheria ya kuwadhibiti waovu. Kwa hiyo, mfumo wa sheria ndio mfumo wa wazi na mpana wa utoaji haki na ambao umebaki kuwa tumaini katika mataifa.

Watawala wanaosimamia mfumo wa sheria wasipokuwa watu wa haki, hutumbukiza taifa zima katika mfumo wa uovu.

Kwa upande mmoja, ni muhimu kukumbusha mihimili kama Bunge juu ya ulazima wa kujenga dhamira safi katika kutunga sheria. Sheria za haki hutungwa ili kulinda mambo yaongezayo amani na furaha ya taifa na kuzuia mambo yaondoayo amani na furaha yao.

Bado hatujasahau mchakato wa kupata katiba mpya Tanzania ulivyokwenda



*Jaji Mkuu wa Tanzania Prof. Ibrahim Juma*

wakati ule na jinsi tunavyoendelea kupigana mateke juu ya jambo hilo.

Tunaliombea Bunge kwa sababu ndipo inapotakiwa kukaa hekima ya kuona na kutunga sheria zinazoletea baraka taifa.

Yawezekana zikawepo sheria nzuri, lakini vyombo vinavyosimamia ufafanuzi na utekelezwaji wake vikawa vimegubikwa na uovu.

Kwa sababu hiyo, haki haitolewi ipasavyo na inapotolewa hutolewa kwa kupindisha sheria na hukumu. Dhamira safi katika kutawala na kusimamia utoaji haki ni chimbuko la baraka na fahari ya taifa.

Sheria nzuri katika taifa ni msingi wa baraka. Usimamiaji wake ukiwa mzuri ni baraka juu ya baraka na pia ni fahari kwa taifa. Usimamiaji mbaya hupeperusha bendera ya uovu na hivyo kuliletea taifa laana na aibu.

Haki ni chimbuko la amani na furaha ya kila mtu. Haki ni nguzo ya kati inayoshikilia baraka na fahari ya taifa.

Pasipo Haki hakuna maendeleo ya kweli! Bunge, na watawala, na mahakama kwa dhati wakijifunga mshipi wa Haki ndipo baraka itakuja juu ya taifa letu mpaka tushangae.

---





**Na Evarist Chahali**  
evarist@chahali.com

## **Tujadili kumomonyoka maadili yetu**

**K**ATIKA makala yangu moja ndani ya gazeti hili nilizungumzia kuhusu kuzagaa kwa vitendo vya ulawiti nchini Tanzania, na nikahitimisha kuwa suala hilo linachangiwa zaidi na unafiki miongoni mwa Watanzania.

Kwa bahati mbaya, makala hiyo ililisababishia matatizo gazeti hili. Mzungu mmoja anayefuatilia mambo mbalimbali ya Tanzania aliliripoti gazeti hili kuwa linachochea chuki dhidi ya watu wanaojihusisha na “mchezo” huo, akitolea mfano makala yangu hiyo.

Nilikerwa sana na kitendo cha mzungu huyo kwa sababu kadhaa, kubwa ikiwa aliamua kwa makusudi kupotosha lengo la makala hayo.

Kadhalika, kwa vile anafuatilia mambo ya Tanzania kwa karibu, naamini bila shaka anafahamu kwamba sheria, mila na desturi za nchi hiyo zinaharamisha mambo hayo.

Tatizo ni kuwa wapo baadhi watu wana akili za kikoloni zinazochangiwa na ubaguzi wa rangi, ambapo wanaamini ni wao tu wenye haki ya kuongelea masuala ambayo hata kama hayawahusu.

Na mara nyingi wanafanya hivyo kwa nchi zetu masikini tu lakini wakienda nchi zinazojitweza kiuchumi kama za Uarabuni, wanaufyata.

Nimegusia tukio hilo kwa sababu makala haya inahusu video moja iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii wiki iliyopita ambapo watoto wanafunzi wa shule moja ya msingi jijini Dar es Salaam walikuwa wanaeleza jinsi wanavyolawitiana.

Kuna vitu kadhaa vya kusikitisha kuhusu video husika. Kwanza, umri wa watoto hao ni wastani wa miaka 10 hivi,



**Wasiri wa Maendeleo ya Jamii na Jinsia  
Doroth Gwajima**

lakini ndio wameshajiingiza kwenye vitendo hivyo vya kishoga.

Pili, walimu waliokuwa wakiwahoji na kuwarekodi walisikika wakitumia lugha isiyofaa hata kidogo, na wala hawakuona umuhimu wa kuziba sura za watoto husika.

Lakini pengine kilichokera zaidi ni ukweli kwamba hakuna kiongozi yeyote wa serikali, chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM) au chama chochote cha upinzani aliyeongea lolote kuhusu suala hilo.

Hata hivyo, pengine kuwalaumu viongozi hao ni kuwaonea kwani hata mapokeo ya wananchi wa kawaida yamekuwa duni. Ni watu wachache tu walioonekana kuguswa na kilichomo kwenye video hiyo.

Watu wachache waliotoa maoni yao kuhusu video hiyo waliwatupia lawama wazazi na kueleza kuwa msingi wa maadili mema ni katika ngazi ya familia. Walidai kuwa wazazi wengi “wapo bize” na majukumu mengine kiasi cha kutowekea mkazo malezi bora kwa watoto wao.

---

## **Samia kuvuna kura za vijana, wanawake, wapinzani**

*Inatoka Uk. 4*

kupiga kura.

Anasema tatizo kubwa la ajira kwa Tanzania liko kwa vijana zaidi na kwamba walikikimbia kilimo kwa kuwa hakukuwa na kitu kinachowavutia na kwamba serikali ilionekana “kukitelekeza” kilimo kwa muda mrefu.

“Kila mara tunaelezwa kilimo ni uti wa mgongo wa Tanzania, lakini serikali ni kama ilikuwa inadanganya, hakuna uwekezaji, hakuna miundombinu inayofaa, hasa huko kunakofanyika kilimo, hivyo hatua ya sasa kuonyesha Rais Samia, amekishikia bango kilimo, kutawavuta vijana wengi kufanya kazi za kilimo,” anaongeza dajitari huyo wa uchumi ambaye taasisi yake inajihusisha na utafiti.

Daktari huyo anapongeza hatua ya Rais Samia kuwaweka wanawake pia katika mipango ya kilimo na biashara zingine ndogondogo kwani kufanya hivyo kutawainua kiuchumi na kuwa na maana halisi ya “walezi wa familia.”

Katika mpango wake wa kuwanufaisha vijana na wanawake, Rais Samia ametangaza kwamba serikali itawawezesha vijana kupitia umiliki wa ardhi na kwamba mchakato huo ndiyo kipaumbele kikubwa cha serikali ya awamu ya sita.

Kwa ajili ya kufanikisha lengo hilo, tayari serikali imetenga hekta 680,000 kwa ajili ya wanawake na vijana, wenye nguvu za kuzalisha chakula cha kutosha na kuuza ziada nje ya nchi.

“Serikali imetenga hadi ekari 10 kwa kila kijana mwenye sifa ambapo baadaye watazimiliki,” amesema Rais Samia, ambaye anaonekana kuilenga nguvukazi ya vijana, wenye kuunda asilimia 45 ya watu wote, kama injini ya mabadiliko ya kiuchumi kupitia sekta ya kilimo.

Rais Samia anasema serikali iko katika mchakato wa kupokea maombi kwa kundi la kwanza la vijana watakaopata

fursa ya kupata mafunzo ya miezi mitatu kuanzia katikati ya mwezi Februari halafu wagawiwe ardhi.

Katika kuipa nguvu na uhai zaidi ajenda ya Rais Samia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imekubali kuipatia Tanzania mkopo wa dola za Marekani milioni 120 ajili ya sekta ya kilimo ikiwemo umwagiliaji na kujenga kituo cha usafirishaji na usambazaji mboleo.

Sehemu ya mkopo huu itatumika kwa ajili ya kuanzisha “Mfuko wa Pembejeo kwa ajili ya Dhamana kwa Vijana na Wanawake,” yaani “Agricultural Input Trust Fund.” Fedha katika mfuko huu zitatumika kuanzisha vituo atamizi kwa ajili ya mafunzo ya vijana, yaani “incubation centres.” Pia zitatumika kuwawezesha vijana na wanawake kupata mikopo kwa ajili ya mbolea, dawa za kuua magugu na wadudu.

### **Mpango wa BBT**

Katika kuhakikisha kwamba malengo ya serikali yanatimia, serikali – kupitia Wizara ya Kilimo imeandaa mpango madhubuti unaolenga vijana na wanawake ujulikanao kwa jina la BBT, yaani “Ujenzi wa Kesho Bora.

Rais Samia anasema Tanzania imeamua kuanzisha mpango huo kutokana na idadi kubwa ya vijana kukosa sifa zinazohitajika na taasisi za kifedha wanapoomba mikopo, hivyo kupitia mpango huo, wataweza kupata mikopo kwa ajili ya kuendesha shughuli za kilimo.

Pambazuko lina taarifa kwamba tangu kuanzishwa kwa mpango huo wa BBT miezi sita iliyopita, tayari kumetengwa jumla ya hekta 680,000 kwa nchi nzima na shughuli ya kusafisha mashamba hayo imeanza.

Kwa mujibu wa andiko la mradi wa BBT, yaani “Building Better Tomorrow (BBT)” kwa Kiingereza, lililoko kwenye

## **Samia kuvuna kura za vijana, wanawake, wapinzani**

### **Inatoka Uk. 10**

tovuti ya Wizara ya Kilimo, mradi huu utaotekelezwa kwa miaka nane, tangu 2022 hadi 2030.

Andiko linataja nadharia ya mabadiliko, kaulimbiu, shabaha, malengo, madhumuni, mafukumu, vigezo vya kupima kasi ya ufanisi, na limetaja rasilimali zinazohitajika.

Takwimu zinasema kuwa, asilimia 51 ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi na wanaoshughulika na kilimo ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 24. Hawa hulazimika kufanya kazi katika miradi ya wazazi wao, hasa mashambani, kutokana na changamoto ya kuanzisha miradi binafsi ya kilimobiashara kwa sababu kadhaa.

Sababu hizo ni pamoja na ukosefu wa ujuzi na stadi za kazi; ukosefu wa ardhi; ukosefu wa mtaji wa kifedha; ukosefu wa masoko; ukosefu wa hamasa ya kujiajiri katika kilimo kwa sababu ya fikra kwamba kazi ya kilimo sio mradi unaoweza kuleta tija stahiki kwa wakati mwafaka; na ukosefu wa mfumo wa kuratibu juhudi za vijana walio tayari kwa ajira karika sekta ya kilimo.

### **Bajeti ya mradi wa BBT**

Bajeti kamili ya mradi iliyotajwa kwenye andiko ni Shilingi za Tanzania bilioni 356.199, sawa na dola za Marekani 148,416,167. Asilimia 24 ya fedha hizo itatokana na bajeti ya Wizara ya Kilimo na TAMISEMI. Na asilimia baki 76 itatoka kwa wadau wa maendeleo, azaki, na makampuni ya sekta binafsi.

Mchanganuo wa jumla wa bajeti hii ni kama ifuatavyo: Eneo la kwanza, yaani kuhamasisha vijana na wanawake (“inspire”), limetengewa shilingi za Tanzania 7,645,000,000; sawa na asilimia 2.1 ya bajeti yote.

Eneo la pili, yaani kuwezesha upatikanaji wa ujuzi na ustadi wa kazi (“empower”), limetengewa shilingi za

Tanzania 241,680,000,000; sawa na asilimia 67.8 ya bajeti yote.

Eneo la tatu, yaani kuwezesha upatikanaji wa mitaji na masoko (“engage”), limetengewa shilingi za Tanzania 86,694,000,000; sawa na asilimia 24.3 ya bajeti yote.

Eneo la nne, yaani kuwezesha utendaji kazi katika mazingira yaliyo rafiki kiseri na kisheria (“enable”), limetengewa shilingi za Tanzania 1,368,000,000; sawa na asilimia 0.4 ya bajeti yote.

Na eneo la tano, yaani muundo wa usimamizi wa mradi (“coordinate”), limetengewa shilingi za Tanzania 18,811,800,000; sawa na asilimia 5.3 ya bajeti yote.

### **Kuvuna wapinzani**

Mbali na nguvu inayowekezwa kwenye kilimo, hasa kupitia kwa vijana, wachambuzi wanaeleza kwamba upo uwezekano mkubwa kwa Rais Samia “kuzoa” kura nyingi kutoka kwa wanachama na mashabiki wa vyama vingine vya ushindani.

Kwamba kufungua milango na kupungua zuio la kukataza mikutano ya hadhara lililowekwa na mtangulizi wake, John Magufuli kwa kipindi cha miaka sa, kunampa fursa ya kupendwa na hata waliokuwa vyama vikubwa vya ushindani; hasa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), NCCR-Mageuzi, ACT-Wazalendo.

“Pamoja na kuonekana hana makeke wala mbwembwe za uongozi, Rais Samia kwa hatua anazochukua kuiweka nchi katika misingi ya usawa na haki kwa kila mmoja, anavuna idadi kubwa ya wapinzani wake, hawa nao watakuwa wapigakura wake kwenye uchaguzi mkuu ujao, “anasema Obadia Kisonge, ambaye amejitambuisa kwa Pambazuko kuwa ni mwanachama wa ACT-Wazalendo. Anaongeza; “weka maneno haya benki na nikumbushe 2025.”

## Twitter kumkutanisha Samia, Vivian

Na Mwandishi WETU

**M**TANDAO wa kijamii, Twitter umethibitika kurahisisha mawasiliano miongoni mwa watu duniani bila kujali rangi, rika, dhamana na hata umbali.

Sasa imedhihiria kuwa kupitia mtandao huo, Rais wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan atakutana na kujadili masuala mbalimbali yanayohusu afya na mtaalamu wa sekta hiyo, Vivian Joseph.

Vivian hakuhitaji kupitia itifaki ngumu na pengine kuchukua muda mrefu zaidi kukutana na kiongozi wa nchi – na huenda kukataliwa na wasaidizi, bali kwa andiko lake la maneno 44 kwenye Twitter, lilitosha kumuibua Rais Samia ambaye alijibu kupitia mtandao huohuo wa kijamii na kuandika; “nawaagiza wasaidizi wangu wapange namna na siku ya kukutana nawe.”

Akiwa anaadhisha tarehe moja ya



**Rais Samia Suluhu Hassan**

“Ninasherehekea siku yangu ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwangu na Mheshimiwa Mama Rais Samia Suluhu. Ninatamani siku moja kwa mwaka huu kuzungumza naye kuhusu masuala yanayogusa afya katika ukanda wa SADC. Nitafarijika zaidi ikiwa hili litafanyika. Heri kwa siku yako ya kuzaliwa. Heri kwangu pia kwa siku ya kuzaliwa.”

Baada ya saa 11 hivi, Rais Dkt. Samia alimjibu Vivian kwa Kiingereza (Tafsiri ya Kiswahili siyo rasmi); “Heri ya siku ya kuzaliwa kwako Vivian. Aksante kwa kunitakia heri. Wasaidizi wangu watakufikia ili kupanga namna ya kukutana na kuzungumza nawe.”

“Ni nadra sana kwa kiongozi mkuu wa nchi kuwasiliana moja kwa moja na mwananchi wa kawaida, tena ambaye anaomba miadi na kukubaliwa kupitia mtandaoni, ni faraja kubwa kuona Rais Samia amejibu na kukubali kukutana na Vivian,” anaandika Jamillah Heri kwenye ukurasa wake wa Twitter.

Ijumaa iliyopita – Januari 27, Rais Samia alitimiza miaka 63, huku Vivian – mwanaharakati kijana kuhusu afya ya mtoto, akifikisha miaka 29. Vivian pia ni Mkuu wa Dawati la Afya (hasa kwa vijana) ndani ya Jumuiya ya Uchumi Kusini mwa Afrika (SADC).



siku ya kumbukumbu ya kuzaliwa na Rais Dkt. Samia; Januari 27, Vivian aliandika katika Twitter yake akimpongeza kiongozi huyo wa Tanzania kwa kusherehekea siku yake muhimu – ya kukumbuka kuzaliwa kwake, huku akieleza matamano ya kukutana naye.

Vivian aliandika kwa Kiingereza (na hapa ni tafsiri isiyo rasmi ya Kiswahili);



## Mwenye haki ndiye mwenye nguvu

Na **Beneditt MSOFFE**

**K**ATIKA ulimwengu wa haki, kanuni kwamba “mwenye haki ndiye mwenye nguvu” hutawala. Lakini katika ulimwengu wa kibabe, kanuni kwamba “mwenye nguvu ndiye mwenye haki” hutawala.

Katika kitabu cha Biblia lipo simulizi maarufu lenye kuonyesha ubaya wa kanuni kwamba “mwenye nguvu ndiye mwenye haki.” Ni simulizi la Mfalme Herode Antipas dhidi ya Yohane mbatizaji (Mathayo 14:1-12).

Simulizi hili linazungumzia uamuzi wa Mfalme Herode wa Uyahudi kumuua Yohana.

Katika kitabu cha Walawi sura ya nane, lilikuwa ni kosa mtu kumwoa mke wa mdogo wake. Hata hivyo, Herode alivunja sheria hii. Alimwacha mkewe na kumwoa Herodia, mke wa mdogo wake

Yohana aliamua kumkemea Mfalme Herode. Na Herodia akamchochea mumewe Herode hadi akamtia Yohana gerezani.

Katika sikukuu ya kuzaliwa kwake Mfalme, binti yake alicheza vizuri mbele yake naye Mfalme akamuahidi kumpa zawadi yoyote aipendayo.

Binti kwa kuelekezwa na Herodia, mama yake, aliomba kichwa cha Yohana. Mfalme hakutarajia ombi la ajabu namna hiyo. Lakini ili kutunza ahadi yake alitekeleza na hivyo ndivyo mauti ilivyomkuta Yohana.

Tukio hili linafanana na maovu mengi ya siku hizi. Yohane aliamua kuitetea sheria kwa kumkemea Herode. Huu ni pendo kwa herode. Lakini, badala ya Herode kujirekebisha, alichagua kumuadhibu Yohane kwa sababu ya kumweleza ukweli.

Herode hakujua kuwa uovu mmoja unaonyamaziwa au kushangiliwa leo, kesho utazaa uovu mwingine Zaidi, hata kama ni kumwaga damu ya mtu asiye na hatia.

Yaliyotokea enzi za Herode yanatendwa



Njiwa

na mwanadamu wa leo ambaye mara nyingi huchagua kumwagamiza mtu anayemjali kwa kumrekebisha.

Anayekemea anabambikwa ukosaji na mkosaji anawekwa huru. Anayetetea sheria anaadhibiwa na anayekiuka sheria anatembea mitaani kifua mbele.

Kusudi kuchukua msimamo kama aliouchukua Herode, mwanadamu huendekeza kiburi chake. Badala ya kushughulika na kujirekebisha, anaamua kukivunja kioo kinachomwambia ukweli wa namna alivyo.

Na tabia hii imevunja urafiki mwingi, ndoa, undugu, mahusiano katika kazi na hata kudhoofisha ustawi wa kisiasa na kimaendeleo katika mataifa mengi.

Lakini, Agano la Kale linatwambia kwamba, kati ya vitu dhahiri anavyovichukia Mungu ni pamoja na macho ya kiburi, ulimi wa uongo na mikonono imwagayo damu isiyo na hatia, (Mithali 6: 16 - 17).

Na Agano Jipya linasema kuwa, ukweli pekee ndio kitu chenye uwezo wa kutuweka huru (Yoh 8:32).

Kwa hiyo, somo kubwa hapa ni kwamba, mwisho wa kanuni kwamba “mwenye nguvu ndiye mwenye haki” ni mbaya siku zote. Watawala wetu wa kidini na kiraia wanapaswa kuepuka kanuni hii.

Badala yake, kanuni kwamba “mwenye haki ndiye mwenye nguvu” itawala mioyo ya viongozi wetu.

**Mbunge wa Chalinze ziarani**



*Mbunge wa Jimbo la Chalinze, Ridhiwani Kikwete hivi karibuni alifanya ziara ya kutembelea wananchi katika jimbo lake. Katika picha hizi anaonekana akiwa na watoto wenye uhitaji maalum wa Shule ya Msingi Chalinze na kituo cha kulelea watoto wenye uhitaji maalum katika Kijiji cha Kuleana Chalinze. Misaada aliyopelekwa kwa watoto hao ni pamoja na sare za shule, mabegi, viatu, soksi na nguo za kushindia nyumbani. (Picha na Ofisi ya Mbunge).*



# **Pambazuko**

**SASA  
TUNAPOKEA  
MATANGAZO**

**EWE  
MFANYABIASHARA  
NA MTOA HUDUMA,  
ENDAPO UNAHITAJI  
KUWAFIKIA WATEJA  
WENGI ZAIDI BILA  
KUJALI MIPAKA YA ENEO  
ULILOPO, TANGAZA  
NASI KWA**

Kuwasiliana kupitia: 0744 768 263  
au Barua- Pepe; [info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz)

## **Samia aache alama kwa kubadili Katiba**

**Na Revocatus KUULI**

**N**IMEFARJIKA kwa uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuonyesha dhamira yake kupanua, kuimarisha na kuhakikisha demokrasia inakua.

Nia ya Rais Samia kuona wananchi wake wanapata fursa ya kufurahia matakwa ya kikatiba na sheria yameleta furaha kwa wengi na siyo wanasiasa tu, bali umma wa Watanzania.

Mtazamo wa Rais Samia kwamba upo umuhimu wa kuzifanyia marekebisha baadhi ya sheria zinazohusika na siasa ikiwa ni pamoja na Sheria ya Uchaguzi Ibara ya 343, unaleta faraja zaidi na kuweka nia yake njema kwenye mizani ya “mzalendo wa kweli.”

Sheria zetu ya uchaguzi zimekuwa zikilalamikiwa sana na wadau mbalimbali wa siasa kuwa zinaminyia demokrasia nchini, lakini pia sheria hizo zinazonekana kukiuka baadhi ya vifungu katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mambo yanayolalamikiwa ni pamoja na matokeo ya uchaguzi wa rais kutopingwa mahakama, hivyo kupingana na haki ya mtu kudai haki yake mahakamani pale mtu huyo anapoamini uchaguzi huo haukuwa huru na haki, hivyo kuhitaji msaada wa mahakama kupata haki hiyo.

Haki ya mtu kuchagua na kuchaguliwa ni suala linalotia ukakasi katika sheria, wakati kupiga kura au kupigiwa kura ni haki ya msingi katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria ya Uchaguzi inaweka masharti kwa mgombea kuwa mwanachama wa chama cha siasa ili kupata sifa za kuchaguliwa huku ikitoa nafasi ya kupiga kura au kuchagua kwa kila Mtanzania mwenye umri unaoruhusiwa – miaka 18 na kuendelea.

Haileti mantiki kumpa mtu haki ya kuchagua bila kujali uanachama wake kwa chama chochote, lakini sheria hiyohiyo ikaona mantiki ya ulazima wa mtu anayechaguliwa kuwa mwanachama



**Kuuli**

wa chama fulani na hivyo kuwanyima wanachi wasiokuwa wanachama wa vyama vya siasa haki yao ya msingi ya kuchaguliwa (kupigiwa kura).

Inasikitisha zaidi kuwa licha ya mahakama kutoa uamuzi unaoruhusu mgombea binafsi katika kesi maarufu ya Mchungaji Christopher Mtikila dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, bado haki hiyo imeendelea kukataliwa kama siyo kupuuzwa.

Kuna suala la mgombea wa kiti cha urais kutangazwa mshindi kwa wingi wa jumla wa kura (simple majority), kwa namna sheria ilivyo sasa ni rahisi kumpata rais aliyekataliwa na watu wengi kuliko waliomchagua kwa mfano rais akapata asilimia 30 huku asilimia sabini zikichukuliwa na wagombea urais wengine.

Inawezekana wagombea hao wengine wamepata asilimia kubwa zikiwekwa pamoja, lakini kila mgombea kati yao hakufikisha asilimia 30 za mshindi.

Hivyo ni vyema kuwepo haja ya kumpata mshindi wa urais kwa asilimia zaidi ya 50 kwa kubadili Katiba na sheria ili mshindi wa kiti cha urais apatikane zwa zaidi ya asilimia 50 ya kura zote.

Na ili kuondokana na kanuni ya mshindi kwa kura za jumla (simple majority rule) ni muhimu Katiba na Sheria ya Uchaguzi zikaruhusu vyama



## **Samia aache alama kwa kubadili Katiba**

*Inatoka Uk. 16*

kushirikiana kupata ushindi kwa kuruhusu vyama vya siasa kuungana kwa lengo la kupata ushindi katika uchaguzi (political parties coalition) au kuruhusu vyama kushirikiana kuunda serikali (Coalition Government), hali hii itasaidia kuimarisha demokrasia, kukaribisha ushirika wa kisiasa baina ya vyama vya siasa.

Kubwa zaidi ni muundo wa Tume ya Uchaguzi ambao kwa hakika unaleta ukakasi katika kusimamia na kutoa haki kwa wagombea wa vyama vyote.

Kwamba tume hiyo kuwa na makamishna wake wanaoteuliwa na mmoja wa wagombea au chama chake, kunaonekana wazi kuwepo kwa mwanya wa kutotenda haki.

Hivi kwanini wasiwepo makamisha na watendaji wengine wa tume hiyo ambao wanaajiriwa – baada ya kupitishwa kwenye mchakato mkali na wenye uwazi katika usaili; kuanzia makamishna hadi maofisa wake wengine hadi ngazi ya kata au kijiji.

Pia tume kuendelea kuwatumia maofisa wa serikali, wakurugenzi wa halmashauri kuwa wasimamizi wa uchaguzi kwenye maeneo yao, siyo sahihi kabisa.

Wakurugenzi wa halmashauri ni waajiriwa wa serikali ambayo inasimamia utekelezaji wa ilani na matakwa mengine ya chama kinachokuwa madarakani, sasa kuna nafasi finyu zaidi ya watendaji hao kutenda haki dhidi ya vyama vingine vinavyowania kuingia madarakani wakati yeye akitakiwa kusimamia haki na kutenda kwa usawa.

Halafu suala la mbunge anapohama chama wakati akiwa anatumikia nafasi hiyo, kwamba anapoteza nafasi yake, halijakaa sawa na linavunja Katiba kwa kuwa huyu ni mwakilishi wa wananchi na kamwe siyo chama, kwenye chama “amepitia” tu kwa mujibu wa Katiba.

Hivyo, ni vyema mbunge anapohama chama asipoteze ubunge na hata



**Mwanasheria Mkuu wa Serikali Jaji Dk. Elieser Mbuki Feleshi**

anapofukuzwa, abaki na dhamana hiyo kwa kuwakilisha waliomchagua. Sheria ya sasa inamfanya mbunge aliyechaguliwa kuwa mwoga kwa chama chake na siyo kwa waliomtuma kwenda kuwakilisha.

Na pia kuwepo uwezekano wa mbunge “kuwajibishwa” na waliompigia kura wakati wowote na isiwe kusubiri miaka mitano ndipo aondolewe kwa kura.

Mbadiliko haya yakifanyika, upo uwezekano mkubwa kwa Tanzania kuwa kinara wa demokrasia na utawala bora Afrika – huku wananchi wake wakipata fursa ya kufurahia matunda ya kuheshimiwa na viongozi walioko madarakani.

Pamoja na yote haya, ni vyema zaidi kukawepo sheria moja muhimu ya masuala ya uchaguzi kwa kuziungansha Sheria ya Uchaguzi ya Taifa - aya ya 343 na ile ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa - aya ya 292.

Inawezekana Rais Samia akawa ndiye “kinara” aliyekuwa akisubiriwa kuibadili nchi na kuwa na Tanzania yenye kila aina ya heri na faraja kwa wananchi wake.

Kuuli ni wakili ICC, IRMCT, AfCHPR, Mahakama Kuu Tanzania, Mahakama Kuu Zanzibar, Mkurugenzi wa Halmashauri (mstaafu) na Msimamizi wa Uchaguzi. Sasa ni Wakili wa Serikali Mkuu-Wizara ya Katiba na Sheria.

---

## Maana, aina na vyanzo vya maarifa

Na Shabaan LULELA

**K**ILA binadamu ni kiumbe mwenye kuwezo wa kufikiri, kupanga, kuamua na kufanya matendo huru. Huu ni mchakato wa kukusanya, kuchakata, kutunza na kutumia maarifa ikiwa ni msingi wa mipango na matendo.

Je, “maarifa” ni kitu gani, sio kitu gani, na binadamu hupataje maarifa hayo?

Kitabu, “The Oxford Handbook of Epistemology (2002),” kilichohaririwa na Paul Moser, kinatusaidia jawabu. Nakitumia kujadili maana, aina na vyanzo vya maarifa.

Maarifa ni taarifa zilizo kichwani mwa mtu fulani, kuhusu jambo fulani, katika wakati fulani, na ambazo ukweli wake unaaminika kwa sababu zina ushahidi thabiti.

Lakini, pasipo ushahidi thabiti taarifa hizo zinabaki ni tetesi tu. Mfano, tamko kwamba: “Juma anajua kwamba Neema yuko Zanzibar,” linaweza kuwa maarifa ya kweli au tetesi ambazo ukweli wake haujathibitishwa.


Kuna njia kuu tano za kuvuna maarifa na kuyahifadhi kichwani. Mosi, ni utambuzi unaofanyika kwa kutumia milango mitano ya ufahamu; yaani macho, pua, masikio, ngozi na ulimi kudaka taswira za vitu vilivyo katika mazingira ya mtu anayefanya utambuzi (perception).

Milangi mitano ya fahamu hutumiwa zaidi na wanasayansi katika mchakato wa utafiti unaohusisha majaribio.

Pili, ni kwa kujichunguza kimoyo moyo ili kubaini hisia, fikra, njaa, kiu na maumivu ya kimwili (introspection).

Wewe pekee ndiye unayeweza kujichunguza na kujielezea kwa kutumia mtazamo wa nafsi ya kwanza. Hiyo ndiyo maana ya kujichunguza.

Tatu, ni kwa kutumia kumbukumbu za matukio ya muda wa nyuma



**Maarifa**

yaliyohifadhiwa ubongoni mwako (memory). Ubongo wa mtu ni kama mkanda wa kamera. Unapiga picha na kutunza matukio, na “ukichezwa” kwa kurudi nyuma matukio hayo yanakumbukwa.

Nne, ni kwa kutumia ushuhuda wa maneno au maandishi ya watu wengine wanaoaminika kuwa chanzo cha maarifa sahihi, na hivyo mamlaka ya kimaarifa (testimony).

Hapa kuna wazazi, walimu, madaktari, waandishi wa vitabu, misahafu, waandishi wa magazeti, wanasayansi na wanateolojia. Hata mtu anayekwambia “ni muda gani,” au “njia ya kwenda dukani ni ipi,” naye ni shuhuda.

Na tano, ni kwa kutumia uchambuzi na usanifi wa kimantiki (logic). Hapa kuna kujadili mambo kwa kufasili dhana, kulinganisha dhana, kutofautisha dhana, kunyumbulisha dhana, na kusanifu hoja.

Kusanifu hoja ni mchakato wa kimantiki unaofanyika kwa kuanzia ushahidi mchache na kutengeneza hitimisho la ushahidi mwingi (induction); au kuanzia ushahidi mwingi na kutengeneza hitimisho la ushahidi mchache (deduction); au kutumia njia zote mbili (abduction).

Mbinu hizi hutumiwa zaidi na wanafalsafa na wanateolojia. Mfano wa “abduction” huu hapa: Hakuna mzee wa kiume wa miaka 200; Hakuna mzee wa kike wa miaka 200; kwa hiyo watu wote hufa.

## **Ukomo wa maarifa katika akili za watu**

**Na Dkt. Humbe KILISE**

**T**UNAFAHAMU kwamba, binadamu huvuna maarifa yake kwa kutumia njia kuu tano; milango ya fahamu, kumbukumbu, kujichunguza, ushuhuda, na udadavuzi wa kimantiki.

Je, binadamu anao uwezo wa kupata ufahamu wa maarifa juu ya kila kitu kilichopo hapa ulimwenguni?

Professor Colin McGinn, Mwingereza anayeishi Marekani, anatoa jawabu la “hapana,” katika kitabu chake, “The Problem of Consciousness: The Limits of human Inquiry (1991).”

Kwa faida ya wasomaji, napendekeza kufupisha hoja yake hapa chini. Hoja yake inajengwa juu ya dhana kuu ifuatayo:

Kwamba, wadudu, wanyama hayawani na binadamu wana “ubongo” wenye akili, ambacho ni kiungo cha mwili chenye uwezo wa kufanya kazi ya kutambua vitu kwa kupokea taarifa kuhusu taswira za vitu husika, na kuzitafsiri hadi kubainisha vitu hivyo. Hoja inaweza kupewa muundo wa kimantiki ufuatao:

Mosi, uwezo wa “akili” za wadudu na wanyama hayawani una mipaka ya utambuzi (cognitive closure), katika sekta za kimaarifa, kama vile kusoma, kuongea, kuandika, na kuhesabu; wakati uwezo wa “akili” za binadamu hauna mipaka ya utambuzi katika maeneo hayo.

Pili, uwezo wa “akili” za binadamu una mipaka ya utambuzi (cognitive closure) katika sekta za maarifa kama vile kuona usiku, kuona rangi fulani, na kunusa harufu fulani; wakati uwezo wa akili za wanyama kama vile paka hauna mipaka ya utambuzi katika maeneo hayo.

Tatu, na kwa hiyo, kila mdudu, kila mnyama hawayani, na kila binadamu, ana uzio wa maarifa wenye kipenyo kinachobainisha mpaka wa eneo la akili yake (cognitive closure) katika baadhi ya sekta za kimaarifa, ukubwa wa eneo la kimaarifa ukiwa unatofatiana kati ya kiumbe na kiumbe, kulingana na maumile ya viumbe hao.



**Ubongo**

Nne, kama ambavyo falsafa ya uhalisia (realism) inasema, vitu halisi vilivyoko ulimwenguni vinaweza kuendelea kuwepo bila kufahamika kwa binadamu yeyote.

Tano, na kwa hiyo, kama ilivyo kwa wanyama baki, akili ya binadamu wa leo haina uwezo wa kuvuna maarifa ya vitu vyote vilivyoko ulimwenguni.

Yaani, kwa sababu za kimaumbile, akili ya kila binadamu wa leo inao mpaka ya wa akili (cognitive closure) unaomzuia kupokea maarifa kutoka katika eneo lililoko nje ya eneo la uzio wa maarifa ya kibindamu.

Anachosema Colin ni kwamba, akili ya mnyama fulani itakuwa na mpaka wa utambuzi (cognitive closure) unaomzuia kukitambua kitu fulani, endapo mchakato wa kiakili kwa ajili ya kutafsiri taswira ya kitu husika, pale akili hiyo inapokutana na kitu hicho, hupata mkwamo katika jitihada za kung’amua hiyo ni taswira ya kitu gani.

Kwa upande wa binadamu, akili zetu hupata mkwamo wa kimaarifa kama huo katika baadhi ya sekta za sayansi, teolojia na falsafa.

Hivyo, yafaa tutambue sekta hizo ili tujifunze kuisho nazo kwa kuonyesha “unyenyekavu wa kimaarifa” (epistemic humility) kwa sababu hiyo. Je, sekta hizo ni zipi?

---

**Akili za binadamu na upole wa kimaarifa**

Na Hekima MWALUSI

**N**I wazi kwamba, kila mdudu, kila mnyama hawayani, na kila binadamu, ana uzio wa maarifa wenye kipenyo kinachobainisha mpaka wa eneo la akili yake (cognitive closure) katika baadhi ya sekta za kimaarifa.

Pia tunaielewa kwamba, ukubwa wa eneo lililo katika uzio wa kimaarifa hutofatiana kati ya kiumbe na kiumbe, kulingana na maumile ya viumbe hao.

Je, uwezo wa akili za binadamu una mipaka ya utambuzi katika sekta zipi za kimaarifa?

Kwa mujibu wa Colin McGinn (1989), katika makala yake, “Can we solve the mind-body problem?” Anaeleza sababu ya “mpaka wa akili” (“cognitive closure”) za binadamu, kuna vitu anaweza kuvitambua na vingine hatavitambua kamwe hadi anakufa.

Lakini, anasema kwamba, kuna mipaka ya akili ya aina mbili. Aina ya kwanza ni “mpaka wa akili unaoweza kubadilishwa” (relative cognitive closure).

Kwa mfano, mpaka wa akili unaomfanya mtu ashindwe kuona bakteria “unahamishwa” kwa kutumia darubini. Na mpaka wa akili unaomfanya mtu ashindwe kuona nyoya angani “unahamishwa” ama kwa kutumia kionambali.

Na aina ya pili ya “mpaka wa akili” ya binadamu ni “mpaka wa akili usioweza kubadilishwa” (absolute cognitive closure).

Kwa mfano, akili ya binadamu haiwezi kufanya utambuzi kwa njia ya kunusa harufu ya mnyama aliyepita mahali fulani akikimbia dakika tano zilizopita kama anavyofanya mbwa.

Pia, akili ya binadamu haiwezi kutambua “malaika” yuko katika chumba kipi au hayumo katika chumba gani ndani ya nyumba.

Sababu ni rahisi. Kitu yabisi kama vile jiwe kina sifa ya “kutopenyeka,” yaani “impenetrability.” Yaani, kikishakalia mwanya, hakuna kitu kingine kinaweza kukaa katika nafasi hiyo.

**Colin McGinn**

Kwa mfano, ukitumbukiza jiwe katika ndoo yenye maji, maji hayo yanahama kulipisha kwa kupanda juu, wakati jiwe linashuka chini. Yaani, maji na jiwe vina sifa ya “kutopenyeka.”

Lakini, malaika ni roho inayoaminika kuwa na sifa ya “kupenyeka,” yaani “penetrability.”

Yaani, malaika ni kama mawimbi ya sumaku yanayoweza kusafiri kwa kupenya ubao na kukamata msumari ulio upande wa pili wa ubao huo.

Au ni kama mawimbi ya sauti yanayoweza kusafiri kwa kupenya ukuta kutoka chumba cha kwanza hadi chumba cha pili.

Hivyo, wakati jiwe likitumbukia kwenye ndoo iliyo na maji, maji hayo yatapanda, malaika akitumbukia humo maji hayatikisiki.

Ni kwa sababu ya sifa hii, wanasayansi wameshindwa kuwatafiti malaika kwa kutumia mbinu ya kisayansi inayotegemea tofauti kati ya “mazingira ya jaribio” na “mazingira ya kudhibiti taarifa potofu.”

Katika “mazingira ya jaribio” kunakuwa na vitu vinavyochunguzwa, na katika “mazingira ya kudhibiti taarifa potofu,” pia. Lakini, haiwezekani kutumia utaratibu huu kuchunguza kitu ambacho hutujua kiko wapi wakati gani.

Yaani, kwa mujibu wa maumbile yake, binadamu ana milango ya fahamu ambayo haiwezi na haitaweza kutambua sifa za roho kama vile malaika, ikiwemo

## Mtakatifu Paulo alikataza umachiaveli

**Na Deusdedith KAHANGWA**

**M**WAKA 2020, aliyekuwa Rais wa Marekani, Baraka Obama, alihojiwa na mwandishi wa gazeti la The Atlantic na kueleza kwa kuwaonya Wamarekani kuhusu “janga la kimaarifa,” yaani epistemological crisis.

Onyo la Obama lilitokana na ukweli kwamba katika mazingira ya sasa, kumekuwepo na changamoto ambayo hujitokeza pale ambapo jamii hupoteza “uwezo wa kutofautisha kati ya ukweli na uwongo.”

Seti ya sentensi unganifu ambayo imebeba kauli za kweli na kauli za uwongo” huitwa “mkanganyiko,” yaani, “paradox,” “mystery,” au “contradiction,” kwa Kiingereza. Mfano, “Tanzania ni nchi huru na Tanzania siyo nchi huru.”

Lakini, kauli ileile haiwezi kuwa kweli na isiwe kweli wakati ule ule na katika mtazamo ule ule. Sentensi yenye kubeba “mkanganyiko” wa aina hii inakuwa na tatizo la “ukanganyifu,” yaani “incoherence.”

Kwa mujibu wa Obama, “janga la kimaarifa” ni sumu katika “soko huria na mawazo,” na hivyo sumu kwa uhai wa mifumo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Kwa ajili ya kufafanua umantiki wa mtazamo huu wa Obama, na jinsi unavyotuhusu hapa Tanzania, najibu swali lifuatalo: “mkanganyiko ni kitu gani na siyo kitu gani?”

Najibu swali hili kwa kutumia mawazo ya watu wawili. Kuna Alvin Plantinga (1974) na kitabu chake, “God, Freedom and Evil”; na kuna James Anderson (2007) na kitabu chake, “Paradox in Christian Theology.”

Kwa mujibu wa Plantinga (1974), kama tukitumia kigezo cha aina za kauli zinazozalisha mikanganyiko, tunaweza kubainisha mikanganyiko ya aina tatu.

Mosi, ni mkanganyiko unaotokana na ukinzani wa wazi kati ya kauli zilizo ndani



*Biblia Takatifu*

ya seti moja (explicit contradiction). Mfano ni seti ya kauli hizi: “Tanzania iko Afrika’ na ‘Tanzania haiko Afrika’.”

Pili, ni mkanganyiko unaotokana na ukinzani uliofichika kati ya baadhi ya kauli zilizo ndani ya seti moja dhidi ya hitimisho linalotokana na baadhi ya kauli zilizo katika seti hiyo hiyo (proximately implicit contradiction).

Mfano ni seti ya kauli hizi: “Watanzania wote huongea Kiswahili’, ‘Juma ni Mtanzania’, ‘Juma haongei Kiswahili.’”

Wakati kauli ya tatu inasema kuwa, “Juma haongei Kiswahili,” kauli mbili za kwanza, zinazalisha hitimisho kinzani kwamba, “Juma anaongea Kiswahili.”

Tatu, ni mkanganyiko unaotokana na ukinzani uliofichika kati ya mahitimisho mawili yanayotokana na baadhi ya kauli zilizo katika seti moja, au ukinzani uliofichika kati ya hitimisho moja katika seti husika dhidi ya kauli ya kweli iliyo nje ya seti hiyo, lakini yenye uhusiano wa lazima na seti husika (remotely implicit contradiction).

Mfano ni seti ya kauli hizi: “Mungu ni roho” na ‘Mungu aliandika Torati kwa kidole chake.” Kutokana na kauli “Mungu ni roho” inafuata kimantiki kwamba, “Mungu hana mwili.”

Lakini, kutokana na kauli “Mungu aliandika Torati kwa kidole chake,” inafuata kimantiki kwamba, “Mungu ana mwili.” Matamko kwamba “Mungu ana

---

**Mtakatifu Paulo alikataza umachiaveli***Inatoka Uk. 21*

mwili” na kwamba “Mungu hana mwili” yanapingana.

Kwa mujibu wa Anderson (2007), kama tukitumia kigezo cha uwezekano wa kutibika kwa mkanganyiko wa kimantiki unaonekana, kuna aina kuu tatu za mikanganyiko.

Mosi, kuna mkanganyiko halisi na usioweza kutibika kwa kuondoa utata wa kimisamiati, hata baada ya jitihada za kutumia taarifa zote zinazoweza kukusanywa kwa msaada wa akili ya binadamu wa leo (incurable real contradiction).

Mfano ni seti ya kauli hizi: “Kuna duara lenye umbo la mraba’ na ‘hakuna duara lenye umbo la mraba.”

Pili, kuna mkanganyiko usio halisi na unaoweza kutibika kwa kuondoa utata wa kimisamiati, baada ya kutumia taarifa muhimu zilizokusanywa kwa msaada wa akili ya binadamu wa leo (curable apparent contradiction).

Mfano wa pili ni seti ya kauli hizi: “Nina sababu ya kufuatilia afya ya mke wangu’ na ‘sina sababu ya kufuatilia afya ya mke wangu.”

Huu ni mkanganyiko unaotibika kama taarifa zifuatazo zikifichuliwa na msemaji: “Nina sababu ya kufuatilia afya ya mke wangu kwa kuwa najali ustawi wake’ na ‘sina sababu ya kufuatilia afya ya mke wangu anapokuwa yuko mikononi mwa daktari bingwa.” Mkanganyiko umefutika.

Mfano wa pili ni seti ya kauli hizi: “Moja kujumlisha moja ni mbili’ na ‘moja kujumlisha moja ni ni kumi.” Huu ni mkanganyiko unaotibika kama taarifa zifuatazo zikifichuliwa na msemaji:

Nilimaanisha kwamba: “katika kizio cha kumi, moja kujumlisha moja ni mbili’ na ‘katika kizio cha pili, moja kujumlisha moja ni kumi.” Mkanganyiko umefutika.

Na tatu, kuna mkanganyiko usio

halisi na usioweza kutibika kwa kuondoa utata wa kimisamiati, hata baada ya kutumia taarifa zote zilizokusanywa na zitakazokusanywa kwa msaada wa akili ya binadamu wa leo (incurable apparent contradiction).

Huu ni mkanganyiko wenye kuonekana katika seti ya kauli kadhaa kwa sababu ya utata wa misamiati unaotokana na kufichika kwa taarifa za ziada zinazoweza kumaliza utata huo, kama zikipatikana.

Lakini, taarifa hizo haziiwezi kuvunwa kwa kutumia milango ya fahamu kwa sababu ziko nje ya uzio wa maarifa unaobainisha mpaka asilia wa akili ya binadamu wa leo (human cognitive closure).

Kuhusu aina hii, baadhi ya mifano inayotajwa katika fasihi andishi ni: fumbo la hulka ya miungu, fumbo la umwilisho wa Yesu, fumbo la msukumano uliopo kati ya roho na mwili, na fumbo la uhuru wa akili ya binadamu.

Fumbo la hulka ya Mungu linasomeka hivi: “Mungu ni roho tupu; akili ya binadamu haiwezi kutumia milango ya fahamu kutambua uwepe wa roho ya Mungu popote; na akili ya binadamu haiwezi kutambua kuwepo au kutokuwepo kwa Mungu.”

Lakini, kuna binadamu wanatambua kwamba Mungu yupo. Kitendawili hapa ni kwamba: wanatambua? Na hata kama ni kwa kuambiwa, huyo anayewambia alijuaje? Kama ni kwa kusoma maandiko ya mwanahistoria, huyo aliyemandika alijuaje?

Fumbo la umwilisho wa Yesu linasomeka hivi: “Mungu ni roho tupu; Yesu ni Mungu; Yesu ni mwili na roho.” Kauli mbili za kwanza zinamaanisha “Yesu ni roho tupu,” lakini kauli ya tatu inasema “Yesu ni mwili,” wakati mwili ni kinyume cha roho. Kitendawili hapa ni kwamba: inatokeaje Mungu awe mwili na roho?

Fumbo la msukumano uliopo kati

## **Mtakatifu Paulo alikataza umachiaveli**

Inatoka Uk. 22

ya roho na mwili linasomeka hivi: “Mawazo hayachukui nafasi yenye ujazo wowote; mwili unachukua nafasi yenye ujazo maalum;kwa hiyo, mawazo hayawezi kuingiliana na mwili.” Lakini, mawazo yanaongoza matedo ya kimwili. Kitendawili hapa ni kwamba: inatokeaje mawazo yaogozo mwili?

Fumbo la uhuru wa akili ya binadamu linasomeka hivi: Mosi, “mfumo wa ulimwengu ni kama wavu unaounda mtandao wa mafundo ya sababu na matokeo, kila fundo likuwa linawakilisha mtendaji au tukio mmojawapo.”

Pili, “binadamu ni sehemu ya mtandao huu wa sababu na matokeo, akiwa anashiriki kwa njia ya maamuzi na matendo anayoyafanya kwa hiari.”

Tatu, na kwa hiyo, “uhuru wake wa maamuzi unaminywa kwa sababu yeye ni sehemu ya mtandao wa sababu na matokeo.”

Lakini, inaonekana kwamba, uhuru wake wa maamuzi ya kibinadamu na mtandao wa sababu na matokeo unaomzunguka vinasikilizana, kiasi cha mfumo huu kumwachia kiwango cha uhuru anaoutumia katika fikra, maamuzi na matendo yake.

Kitendawili hapa ni kwamba: inatokeaje binadamu apate uhuru huo? Na kama anao ni uhuru kiasi gani, na hasa tukizingatia kwamba, akili yake inao mpaka asilia wa kimaarifa (cognitive closure)?

Na fumbo la usawa wa kimungu kati ya Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu linasomeka hivi; “Mungu Baba anajua kila kitu, anaweza kila kitu, yuko sehemu zote, anapenda wote, yupo milele yote”; na “Yesu na Roho Mtakatifu ni sawa na Mungu Baba kwa kila kitu.”

Lakini, Yesu alipokuwa kwenye mtini alithibitika kwamba hajui kila kitu. Pia Yesu alisema kwamba yeye na Roho



Niccolò Machiavelli

Mtakatifu hawajui kila kitu.

Kitendawili hapa ni kwamba: inawezekanaje kwamba “Yesu ni sawa na Mungu kwa kila kitu” na “Yesu siyo sawa na Mungu kwa kila kitu”?

Huu ni mkanganyiko unaotibika, kwa kuwa ushahidi wa kibiblia wenye nguvu kuliko mapokeo upo. Na hapa natofautiana na kina Anderson (2007).

Wito wangu ni kwamba, wanazuoni mamboleo tusaidiane kusafisha “imani ya jamii” kwa kuwaepusha watu wote na mikanganyiko ya kimantiki inayotibika.

Napendekeza kwamba, taasisi inayoitwa “Kanisa” ni mbinu ya kukuzi na kuhami heshima ya ubinadamu.

Lakini, kama Kanisa linakubali kuwa nyenzo ya kusigina heshima ya ubinadamu linakuwa limeamua kukumbatia “itikadi ya umachiaveli.” Yaani, itikadi kwamba “lengo zuri linaweza kuhlalisha mbinu yoyote, ikiwemo mbinu haramu.”

Hivyo, Kanisa linapaswa kuupinga “umachiaveli,” kwa kuwa “ubaya hauwezi kuzaa wema,” kama Mtakatifu Paulo alivyofundisha.

Kwa hiyo, Kanisa linalokumbatia “itikadi ya umachiaveli” hupoteza uhalali wa kimaadili. Wakati wa Kanisa kujitakatifuza ni sasa.

# HUENDA NIKAWAAJIRI HAWA...



## Pambazuko

*Maisha hayana kanuni maalum. Yawezekana kabisa hawa wanaokwenda shule kupata elimu na baadaye kupata vyeti baada ya kuhitimu, wakaajiriwa na huyu kijana "machinga" anayetembeza bidhaa mitaani na asiyekuwa na elimu. Lakini pia kinyume chake chaweza kuwa kweli. Picha hii imetolewa kwenye intaneti. Mpigapicha wala mahali hakukutajwa, lakini inabeba ujumbe wenye kufikirisha.*

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

